Kujifunza Jinsi Ya Kufanya Kazi Na Watoto Yatima Na Wale Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi

Mradi wa Ustawi wa Jamii kuhusu VVU/UKIMWI unaoendeshwa kwa ushirikiano kwa ajili ya watoto yatima na wale waishio katika mazingira Hatarishi nchini Tanzania

Siku Ya Tisa

Malezi, kusaidia familia, Kuingia kwenye Jamii.

Malezi
Kuzisaidia familia
Kuingia kwenye Jamii

Chanzo:
Henggeler, Scott W. et all (1998). Multi-systemic treatment of antisocial behavior in children and adolescents. New York: Guildford Press.

Mattaini, Mark. (1999). Clinical Intervention with families. Washington, DC: NASW Press.

Malengo

kufikia mwisho wa siku , wasaidizi Ustawi wa Jamii wataweza ku:

- Onyesha stadi muhimu na taarifa kwa ajili ya malezi
- Onyesha aina mbali mbali za malezi na njia za kusaidia walezi na familia zenye watoto waishio kwenye mazingira hatarishi zaidi
- Onyesha muhtasari wa shughuli mbali mbali zinazotajwa katika mwongozo wa kazi
- Eleza jinsi ya kufanya kazi na rasilimali zingine za jamii ili kutetea shughuli na huduma za watoto walio katika mazingira hatarishi zaidi

Malezi

Malezi

- Tumeona ya kuwa ukuaji na maendeleo ya watoto huwezeshwa vizuri zaidi katika mfumo wa familia.
- Kuweka mfumo wa familia kwa watoto Yatima na wale waishio katika mazingira hatarishi mara nyingi ina maana ya kwamba familia zinazotoa malezi ni lazima zisaidiwe katika majukumu yao mapya.
- Ili familia hizi zifanikiwe zinahitaji taarifa na msaada kwa malezi yenye ufanisi, mikakati, haswa kwa watoto ambao hawajawazaa wenyewe.

Malezi

- Kwa hiyo,tunakwenda kushughulikia stadi za malezi.
- Taarifa hizi zinatumika kwa malezi ya watoto wote-wale waliozaliwa katika familia husika na wale ambao wameingi katika hiyo familia baada ya kupoteza wazazi/mzazi .
- Taarifa hii ni ya muhimu haswa kwa malezi ya watoto ambao hawakuzaliwa na huyo mlezi.

Kipimo Cha Malezi: Kutafuta Uwiano Sahihi

ukaribu udhibiti

Ukaribu

- Ukaribu unahusu tabia za maneno na vitendo zenye mwelekeo wa kihisia
  - Hizi ni pamoja na vitendo vya upendo, kukubalika, kumthibitisha mtoto.
- Sauti yenye hisia ambayo mzazi huwasiliana na mtoto inaweza kuwa kati ya ukaribu na kumkataa.
- Wazazi wenye ukaribu huonyesha
- Kiasi kikubwa cha kumkubali mtoto
- Kumlea mtoto
- Matumizi ya maneno mzuri ya kumjenga mtoto

Kukosekana Kwa Ukaribu

- Watoto wanaopata ***viwango vidogo vya ukaribu/upendo*** na ***viwango vikubwa vya kukosa upendo*** wako katika hatari ya kuwa na
  - Matatizo ya kimahusiano na kitabia
  - Ugumu wa kuwaamini watu wengine
  - Maatizo ya kuwa na mwitikio chanya
  - Ugumu wa kuwa mshirikeli kwa wengine

Udhibiti

- Udhibiti humaanisha vitendo anavyofanya mzazi kutoa mwongozo, muundo, Nidhamu kwa mtoto.
- Humfundisha mtoto kutokatatamaa na kuwa mvumilivu.
- Humfundisha mtoto kanuni na tabia zinazokubalika katika jamii
- Kushirikiana na watu wengine
- Kujiepusha na ugomvi
- Kuheshimu mamlaka

Kukosekana Kwa Udhibiti Unaotakiwa

- ***Watoto wanaopitia udhibiti wa ukatili miakakati,tabia zisizo na utaratibu maalumu, na/au kutokuwepo kwa ufuatiliaji wako katika hatari kubwa ya:***
  - Matatizo ya kitabia
  - Uhalifu
  - Kutumia madawa

Aina Za Malezi



Aina Za Malezi

- Utafiti umeonesha kuwa aina ya malezi ambayo imepelekea matokeo mazuri kwa watoto ni malezi yenye miongozo wazi.
- ***Wazazi ambao wako wazi kwa watoto wao, hudumisha:***
  - Kiwango cha juu cha upendo katika uhusiano na watoto wao (Kukubaliwa/kukubalika).
  - Kiwango cha juu cha udhibiti sawia (uongozi, mpangilio, kufuatilia tabia ya mtoto).

Namna Ya Kujenga Malezi Yenye Miongozo Iliyo Wazi

- ***Mawasiliano:***
  - Kumsikiliza mtoto wako.
  - kuwasiliana naye vizuri na kwa uwazi.
- Ushiriki wa watoto katika Jamii.
  - Cheza na mtoto wako
  - Mshirikishe mtoto na wenzie katika shughuli sahihi

Namna Ya Kujenga Malezi Yenye Miongozo Iliyo Wazi

- ***Kutoa Maelekezo muhimu ya kufuatwa na kuelezea madhara yake:***
  - Kuelezea tabia inayotegemewa vizuri
  - Kuanza na zile tabia ambazo ni nzuri
  - Pongezi zitolewe taratibu zinapufuatwa na zisitolewe zikivunjwa
  - Miongozo iweke mahali pa wazi nyumbani ili ionekane vizuri

Namna Ya Kujenga Malezi Yenye Miongozo Iliyo Wazi

- ***Matokeo:*** Kupongezwa na adhabu.
  - Watoto wanatamani sana kupongezwa
  - Watoto wadogo wapongezwe mara nyingi zaidi wanapofuata tabia njema. Pongezi zipungue kadiri umri unavyoongezeka.
  - Kwa vijana wa umri wote, lazima wapongezwe pale wanapofuata tabia nzuri.
  - Pongezi itolewe kwa kufuata taratibu fulani iliyoleteleza tabia inayokubalika.

Namna Ya Kujenga Malezi Yenye Miongozo Iliyo Wazi

- ***Msisitizo:*** Kimsingi binadanamu hutenda kile ambacho ana maslahi nacho. Kwa hiyo, taratibu lazima:
  - Zisisitizwe kwa asilimia mia moja (100%)
  - Zisisitizwe bila upendeleo
  - Mtoto azawadiwe pale anapofanya mema, na anyimwe pale asipofanya vyema au anapovunja taratibu
  - Msifie na sifa iambatane na tuzo
  - Taratibu zikubaliwe na wazazi

Namna Ya Kujenga Malezi Yenye Miongozo Iliyo Wazi

- Ainisha: Kuwa na uhakika wa tabia nzuri na mbaya, hususan zile ambazo mzazi angependa zibadilike.
- Kutunza kumbukumbu: Japo si lazima kuweka kumbukumbu ya kila kitu, lakini pale inapotokea moja ya tabia uliyoianisha inabadilika, ni vizuri kuanza kuweka kumbukumbu.
  - Moja ya mikakati itumikayo hasa ni pamoja na kubandika kumbukumbu za tabia za mwanao nyumbani na kuonyesha alama kutabasamu au nyota kila wakati mtoto anapofanya tabia uliyoikusudia.

Namna Ya Kujenga Malezi Yenye Miongozo Iliyo Wazi

- Epuka malezi ya ukali
  - Epuka viboko
  - Kumpuuza anapofanya kisichopendeza
  - Kuzingatia muda
- Kuwa na ufuatiliaji katika malezi- Kumfuatilia mtoto aliko, anafanya nini, shughuli zake, tabia yake.
- ***Utetezi*** Kushirikiana na wengine kuhakikisha mahitaji ya mtoto anayapata na haki zake zinaheshimiwa.

Mbinu Tatu Bora Zaidiza Malezi.

- Kumshirikisha mtoto katika masuala ya kijamii (Kucheza na mtoto wako na kumshirikisha katika shughuli sahihi)
- Kutoa ufafanuzi sahihi wa maagizo na matokeo yake.
- Kusisitiza mwenendo/ tabia inayokubalika (Fuatilia kile ulichosema)

Kufanya Kazi Na Familia Katika Malezi

- ***Unapo shughulika na familia, zingatia:***
- Aina za malezi
- Visababishi vya Hatari
- Vizuizi vya Hatari
- Uhamasishaji wa aina ya malezi yenye kuleta afya bora
- Kutoa msaada

Kuwajengea Msingi Wa Msaada Kwa Walezi

Changamoto Za Utoaji Huduma Nyakati Zijazo

Kuongezeka kwa idadi ya watu wanaoishi na VVU

Kuongezeka idadi ya watoto yatima na wale waishio katika mazingira hatarishi

Kuongezeka kwa mahitaji ya misaada

Kuongezeka kutegemea walezi

Watoa Matunzo Mara Nyingi…

- Huwajali sana wale wanaowatunza zaidi yao wenyewe.
- Huzisahau afya zao.
- Hawazitumii huduma zilizopo.

Watoa Matunzo Mara Nyingi..

- Huwa na sononi ambayo haijapata suluhisho au ufumbuzi.
- Wanahamasishwa na imani yao ya kiroho katika kuendelea kutoa huduma.
- Hutoa matunzo katika mazingira magumu ya kifamilia.

Wahudumu Huathiriwa Na

- Afya yao wenyewe (ukiwemo UKIMWI)
- Mazingira ya huduma
- Mahitaji na mapungufu ya wanaohudumiwa.
- Majonzi na huzuni kuhusiana na familia, marafiki na wateja wao.

Mwitikio Wa Mtoa Matunzo

- Kutimiza majukumu ya mtoa matunzo.
- Tafsiri mpya ya maisha.
- Msongo wa mawazo na kujihisi kuzidiwa na mambo.
- Simanzi.
- Hasira/chuki.
- Mabadiliko ya kiafya kutokana na mahitaji ya matunzo.

Kukubaliana Na Hali

Kukabili na kushinda:

- Msongo
- Matatizo
- Mambo magumu katika maisha

Uwezo Wa Kukubaliana Na Hali Hutofautiana Kutokana Na

- Utamaduni
- Imani/dini
- Jamii
- Familia
- Asili ya mtu
- Uzoefu

Njia Za Kuwasaidia Walezi

- Kusikiliza na kutatua matatizo
- Kumuunganisha na rasilimali zilizopo.
- Kutumia viongozi wa serikali.
- Elimu, taarifa, mafunzo na warsha mbalimbali.

Njia Za Kuwasaidia Watoa Huduma Za Malezi

- Makundi ya misaada
- Familia au mikutano ya jamii
- Kuwatambua
- Kusaidia kutoa rasilimali kwa ajili ya watoto na familia zao (chakula, makazi/nyumba, matibabu n.k.)

Njia Za Kuwasaidia Walezi Inaendelea

- Kutafuta rasilimali
- Kutambua watubinafsi ambao wako tayari kusaidia na kuwaunganisha na walezi (msaada wa muda mfupi/mrefu.
- Ngazi ya familia
  - Mali za familia k.m. shamba, ardhi, mifugo
  - Mitandao ya Familia ni pamoja na ndugu, marafiki, jirani
- Ngazi ya Jamii
  - Asasi za Kijamii, Asasi za Kidini, mifuko ya fedha ya kijamii, Makundi ya Msaada, Mamlaka za Serikali za Mitaa

Msaidizi Ustawi Wa Jamii Atazisaidiaje Familia Zilizoathirika Na VVU?

- Kutoa matunzo ya kuaminika, endelevu na msaada
- Kubadili mtazamo wa familia kutoka hali ya kukata tamaa kuwa thabiti na wenye matumaini
- Kuendelea kutoa msaada na upatikanaji wa ***tiba, mfumo wa msaada wa kisaikologia*** na ***kijamii***
- Mapambano dhidi ya ***dharau*** na ***kutengwa kijamii*** na kuhakikisha kuwa familia zimeunganishwa kwenye mfumo mzuri wa kutoa msaada
- Ndani ya familia
- Ndani ya jamii
- Ndani ya jumuia kwa ujumla
- Kutoa taarifa sahihi kuhusu VVU na kwa ujumla wake kwa watu walioathirika na walioathiriwa, familia zao na jamii zao

Kazi Za Vikundi Vidogo
Mafunzo Ya Kujenga Stadi Za Kuwasaidia Watoto Na Familia

- Chagua mtu atakayechukua taarifa na kutoa mrejesho
- Majadiliano juu ya masuala ya malezi na msaada kwa walezi- je kuna masuala gani kwenye hivi visa?
- Kufanya kazi kwenye makundi madogo kutengeneza mpango wa huduma na msaada kwa kisa na familia
  - Gawa majukumu kama msaidizi ustawi, mtoto au familia/jirani
  - Fanya igizo dhima kuonyesha jinsi ya kutoa msaada kwa mtoto na familia
- Jadilianeni katika kundi kubwa kuhusu kile mlichojifunza

Tathmini Ya Mwisho Wa Mafunzo

Kifuatacho:

Kuingia Kwenye Jamii

Kuingia Kwenye Jamii

- Jinsi ya Kuingia kwenye Jamii
- Kukutana na viongozi wa kijiji na kufanya mapitio/mrejesho juu ya majukumu ya wasaidizi wa Ustawi Jamii na wajibu wao
- Usimamizi
- Vitendea kazi
- Kuweka mtandao na utetezi
- Kuendelea kuwa na hamasa
- Vyanzo vingine vya usimamizi

Kuingia Kwenye Jamii

- ***Washiriki kujigawa kulingana na kata zao na kujadili yafuatayo:***
- ***Usimamizi:***
  - Jinsi gani ya kupanga kufanya kazi pamoja na msimamizi wako?
  - Nini kitakuwa/mfumo wa utoaji taarifa zako ?
  - Kama huna msimamizi unapangaje kutumia mfumo uliopo?
  - Andaa mpango wa utekelezaji

Kuingia Kwenye Jamii

- ***Vitendea kazi***
  - Namna gani unapanga kutumia mpango wa huduma na fomu za utoaji taarifa
  - Changamoto zipi zinatarajiwa na jinsi utakavyoweza kuzishugulikia?
  - Mwongozo wa kazi
- ***Mtandao na Utetezi***
  - Ni mitandao gani ambayo unapanga kuitumia kwenye kata yako?
  - Je ni kwa jinsi gani utafanya utetezi kwa ajili ya watoto na familia zao?

Mwongozo Wa Kazi

- Kuwafikia na Kuhuhisha/kutambua Watoto waishio katika mazingira hatarishi kwa kushirikiana na wajumbe wa kamati za watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi.
- Jihusishe na watoto waishio katika mazingira hatarishi na familia na watoa huduma
- Tathmini uwezo na mahitaji na toa msaada
- Tengeneza na kuendeleza mpango wa huduma.
- Anzisha mtandao na wadau wengine katika ngazi ya jamii na toa rufaa kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi kwenda kwenye rasilimali nyinginezo

Mwongozo Wa Kazi

- Toa huduma za msingi za ustawi wa jamii kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi, ikiwemo msaada wa kisaikolojia kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi walioathiriwa na kuathirika na VVU/Ukimwi
- Fanya kesi menejimenti na mkutano wa wadau wa kesi
- Tambua rasilimali:Tengeneza orodha ya rasilimali
- Kusanya na weka kumbukumbu ya taarifa/Takwimu kuhusu watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi na washirikishe uongozi wa serikali za mitaa
- Shiriki kikamilifu kwenye mikutano ya kamati za shughuli za watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi

Mwongozo Wa Kazi

- Shiriki katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu haki za mtoto,sheria ya mtoto, sera ya maendeleo ya mtoto na zingine zinazofanana na hizo.
- Kuhamasisha jamii yenu katika ngazi mbalimbali,kuanza na kumudu fedha na rasilimali zingine za watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi
- Kuhudhuria vipindi vya usimamizi na kuendeleza mawasiliano ya kila mara na wasimamizi wenu pamoja na mamlaka za kijiji
- Fanya kazi katika mfumo uliopo wa serikali ya kijiji.

Mrejesho Kuhusu Mafunzo

Sherehe Ya Kufunga Mafunzo